



ACTION 2 DAY PRESS

St. Barbara

The girl who sought the Living God

English · Kiswahili



Long ago, in a shining city by the sea, the sun rose over golden towers and palm trees.

Zamani sana, katika mji unaong'aa kando ya bahari, jua lilichomoza juu ya minara ya dhahabu na mitende.



In a tall castle on a hill lived a little girl named Barbara.

*Katika jumba refu mlimani aliishi msichana mdogo aitwaye
Barbara.*



Barbara looked at the stars and wondered, 'Who made this beautiful world?'

Barbara aliangalia nyota na kujiuliza, 'Nani aliumba dunia nzuri hivi?'



Her father feared new ideas, so he locked her in a tall tower.

Baba yake aliogopa mawazo mapya, hivyo akamfunga kwenye mnara mrefu.



Barbara planted flowers and listened to birds. Her heart stayed full of wonder.

Barbara alipanda maua na kusikiliza ndege. Moyo wake ulijaa mshangao wa uzuri.



A kind priest secretly visited her and told her about Jesus and His love.

Kuhani mwema alimtembelea kwa siri na kumweleza kuhusu Yesu na upendo wake.



Soft light filled the tower as Barbara was baptized. She smiled with joy.

*Mwanga mpole ulijaa mnara wakati Barbara alipobatizwa.
Alitabasamu kwa furaha.*



Barbara asked for three windows — to honour the Father, the Son, and the Holy Spirit.

Barbara aliomba madirisha matatu — kumheshimu Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu.



When her father saw the three windows, he grew angry. She said softly, 'Three lights, one loving God.'

Baba yake alipoona madirisha matatu, alikasirika sana. Akasema kwa upole, 'Nuru tatu, Mungu mmoja wa upendo.'



Her father commanded soldiers to catch her.

Baba yake akaamuru askari wamkamate.



Barbara ran to the mountains and hid in a cave, praying.

Barbara alikimbilia milimani na kujificha pangoni, akiomba.



Where her tears touched the ground, roses bloomed.

Alipomwaga machozi chini, maua ya waridi yakachanua.



A kind shepherd hid her among his sheep.

Mchungaji mwema alimsitiri kati ya kondoo wake.



Soldiers came and asked the shepherd where she went. They found her and took her back.

Askari walikuja wakamuuliza mchungaji alipoenda. Na walimpata na kumrudisha.



Barbara stood brave and said, 'I will never leave my faith.'

Barbara alisimama kwa ujasiri akasema, 'Sitauacha imani yangu.'



Angels shone around her, giving her strength.

Malaika walimzunguka kwa mwanga, wakampa nguvu.



At night, she dreamed of Jesus placing a crown of stars on her head.

Usiku, aliota Yesu akiweka taji ya nyota kichwani mwake.



Barbara forgave everyone — even her father.

Barbara aliwasamehe wote — hata baba yake.



A bright flash filled the sky as her story on earth ended.

Mwangaza mkali ulijaza anga hadithi yake duniani ilipofika mwisho.



Her soul rose like a candle flame to Heaven.

Roho yake ilipaa kama mwanga wa mshumaa kuelekea Mbinguni.



Her tower stood quiet. The three windows glowed softly at sunset.

Mnara wake ulisimama kimya. Madirisha matatu yakang'aa wakati wa machweo.



Now Saint Barbara stands in Heaven, wearing white, holding a tower and palm branch, smiling on the world.

Sasa Mtakatifu Barbara yuko Mbinguni, amevaa nyeupe, akiwa na mnara na tawi la mtende, akitabasamu juu ya dunia.



Painted & edited by

Action2day Art Center · Nairobi

Fabian Romain Lashley
Griffins Nyangaresi Museti
Steve Mugiraneza Rukeramihigo
Caleb Gathii Manyera
Abigael Nyaboke Nyakundi
John Maina Onyango

Irene Kiviya Nduku
Ecclesiastes Madaraka Medo
Kristian Juma Omedo
Maxwell Mukanga Indukule
Angel Miriam Mlenda